HOTUBA YA MHESHIMIWA MAMA SALMA KIKWETE KATIKA TAMASHA LA VIJANA, MRADI WA KUZUIA MIMBA ZA UTOTONI, TAREHE 08 DESEMBA, 2014, LILILOFANYIKA KWENYE VIWANJA VYA OFISI YA WAMA, DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Saidi Meck Sadick, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,

Mheshimiwa Angela Kairuki, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria,

Mheshimiwa Raymond Mushi, Mkuu wa Wilaya ya Ilala,

Mheshimiwa Sofia Mjema, Mkuu wa Wilaya ya Temeke,
Feddy Mwanga, Mwakilishi wa Engender Health,
Wajumbe wa Bodi ya WAMA,

Viongozi wa Serikali na Mashirika mengine,

Walimu na Wanafunzi Wapendwa,

Waandishi wa Habari, Mabibi na Mabwana

Habari za asubuhi.

Awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kujumuika pamoja hapa kwa ajili ya uzinduzi wa kampeni ya "***Jilinde Utimize ndoto yako***".

Kipekee niwashukuru wafadhili wetu, USAID kwa kutoa fedha za kufanikisha mradi huu na Shirika la Engender Health kwa msaada wao wa kitaalam na usimamizi.

USAID wamekuwa washirika wakubwa sana kwa serikali na wananchi wa Tanzania katika juhudi za kutokomeza kabisa maambukizi mapya ya VVU kwa makundi mbalimbali yakiwemo ya vijana. Kwa kweli msaada wao mkubwa ndio uliotuwezesha kuwa na mradi huu ambapo kampeni hii ni sehemu yake.

Hali kadhalika, natoa shukrani zangu za dhati kwa wageni wote mliohudhuria hapa. Uwepo wenu ni muhimu sana katika kuendelea kupaza sauti kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanavuka salama katika kipindi chao cha ujana. Hii ni haki yao na ni wajibu wetu sote kuwaongoza katika kipindi hiki cha mpito.

Wapendwa Wanafunzi, Mabibi na Mabwana,

Ni fahari kubwa kwangu binafsi kuwa sehemu ya mradi huu ambao tayari umeshatoa matokeo mazuri katika maeneo ambapo umekuwa ukitekelezwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Tumearifiwa kupitia takwimu mbalimbali kwamba matukio ya ujauzito mashuleni yameendelea kupungua katika maeneo haya.

Leo tumekutana ili kuzindua kampeni ya *"Jilinde Utimize ndoto yako"*, kampeni ambayo inalenga kutoa hamasa na kuimarisha elimu ya afya ya uzazi kwa vijana wa Tanzania. Malengo ya kampenii hii kwa ujumla ni kuimarisha stadi za kujikinga na mimba za utotoni na UKIMWI miongoni mwa vijana wetu walio mashuleni.

Nawapongeza Engenderhealth na USAID kwa kuona umuhimu wa jambo hili jema na kushirikiana na WAMA kuandaa Tamasha hili kubwa. Mradi huu unachangia katika juhudi za nchi yetu kufikia malengo ya milenia hususan lengo la nne la kupunguza vifo vya akinamama vinavyotokana na matatizo ya uzazi. Ni faraja kubwa kwangu kuzindua mradi huu, na kutumia fursa hii kuwaasa vijana juu ya masuala muhimu ya afya ya uzazi kwa watoto wa kike. Kama wengi mnavyofahamu, masuala ya ustawi wa watoto wa kike ni moja ya mambo ambayo ninayatilia maanani sana. Kwani naamini msingi imara wa afya na elimu kwa wasichana ni muhimu sana katika kupunguza vifo vya akina mama na watoto na hatimaye kuwa na Maendeleo yenye tija kwa taifa letu kwa ujumla.

Mabibi na Mabwana,

Katika kipindi cha miongo miwili sasa, tumepiga hatua muhimu katika kupunguza vifo vya mama na mtoto, lakini bado tunahitaji kuongeza nguvu zaidi kwani matatizo haya huwapata zaidi wasichana wenye umri mdogo.

Katika bara letu la Afrika, moja ya tatu (1/3) ya watu wanoishi kusini na mashariki ya Bara hili ni vijana wenye umri kati ya miaka 10 na 24, na kufikia mwaka 2050 idadi hii inategemewa kuongezeka mara mbili. Hivyo uwekezaji katika elimu ya Afya ya uzazi ni muhimu sana kwa maendeleo ya vijana hawa, ili kuwawezesha kuepuka matatizo mengi kama vile ndoa na mimba za utotoni, unyanyasaji wa kijinsia na magonjwa ya ngono kama ambavyo mmesikia kutoka kwa wawezeshaji wetu wa leo. Takwimu zinaonesha kuwa, zaidi ya wasichana milioni 58 Duniani wameolewa wakiwa na umri wa chini ya miaka 18, na kati ya hao milioni 15 wana umri wa kati ya miaka 10 hadi 14, jambo linalowasababishia kupata matatizo wakati wa kujifungua na wengi wao kupoteza maisha wakati wa kujifungua. Wasichana wadogo pia wamekuwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na wa kingono na kuwasababishia kupata maambukizi ya VVU. Takwimu zinaonesha kuwa duniani kila saa moja kuna maambukizi mapya 50 ya VVU kwa vijana. Hii ina maana kuwa kwa mwaka mmoja kuna maambukizi mapya 430,000. Kwa sasa kuna vijana milioni 2.6 wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

Kwa Tanzania takwimu zinaonesha kuwa wasichana wanajihusisha mapema zaidi katika mapenzi ukilinganisha na watoto wa kiume kwani asilimia 13 ya wasichana wanaanza kufanya mapenzi wakiwa na umri chini ya miaka 15 wakati upande wa wavulana ni asilimia saba tu. Hili ni tatizo kubwa sana na hupelekea wasichana wengi kuacha masomo.

Tunaarifiwa pia kwamba, Msichana mmoja hadi wanne wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 19 wana mimba au watoto. Idadi hii kubwa inaonesha kwamba wasichana wanaendelea kuwa kundi lililoathirika zaidi. Tatizo hili linawasababishia watoto wengi kushindwa kumaliza shule.

Kwa hivyo basi kutokana na hali hii ndio maana tumewaita watoto wa kike kwa uwingi wenu tuzungumze namna gani tunaweza kushirikiana kulipunguza tatizo hili au kuliondoa kabisa.

Wapendwa Wanafunzi, Mabibi na Mabwana,

Sina shaka juu ya umuhimu wa mijadala inayolenga kuboresha afya ya uzazi kwa vijana. Wataalam wanatuarifu kwamba ikiwa hakuna hatua zitakazochukuliwa, maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa vijana yataongezeka sana. Muhimu kabisa ni kuwa vijana wa Tanzania wanatakiwa kupewa elimu ya stadi za maisha, afya ya uzazi na usawa wa jinsia ambayo itaendana na mila na desturi zetu, ili waweze kuwa na uchaguzi na maamuzi mazuri ya maisha yao. Tanzania ya baadaye itategemea jinsi tutakavyowaandaa vijana kujenga maisha yao sasa. Kama wazazi, walimu na walezi wa watoto hawa, tunaowajibu mkubwa, kwanza kabisa kuwa mfano na kigezo kizuri cha kuigwa; kutoa malezi na huduma rafiki na bora; kuepuka mila na desturi zinazochangia tabia hatarishi; kujenga na kusimamia nidhamu na kuzungumza na watoto na kuwapa elimu ya afya ya uzazi na stadi za maisha.

Ikiwa tutawaona watoto wote kama ni wanetu, hatutaweza kuwaacha wakakosa elimu kwa ajili ya ujauzito, wakapata magonjwa ya kingono, wakapoteza maisha kwa kuzaa katika umri mdogo, wakaambukizwa VVU.

Wapendwa Wanafunzi (Wanangu)

Kwa watoto wetu wapendwa, nawaasa kutambua hazina kubwa mliyo nayo kama vijana wa nchi hii. Pamoja na wajibu mkubwa ambao wazazi na walezi wenu wanao, bado jukumu la kujilinda mnalo nyie wenyewe.

Jambo muhimu kuliko yote ni kujitambua kuwa wewe ni nani na kwamba umekuja Duniani kwa wajibu fulani na hakuna mbadala wako. Ukiweza **kujitambua** bila shaka **utajithamini** na utaona umuhimu wa **kujilinda.** Hivyo basi nawaachieni hizo J3 ziweze kuwaongoza kama dira yenu; **J**itambue, **J**ithamini na **J**ilinde.

Ni muhimu sana mjiwekee malengo yenu ya maisha na kujiwekea mikakati ya kufikia malengo hayo. Bila shaka moja ya mikakati ni kuepuka mazingira na tabia hatarishi ambazo zinaweza kukuongoza/kukuelekeza katika ngono. Ni lazima mjitahidi kwa kila hali kuepuka vishawishi rika na vishawishi vinginevyo. Usikubali kupewa zawadi na watu usio na uhusiano wa nyumbani kwani hazitakuwa na faida yoyote isipokuwa kuharibu maisha yako. Maisha yako yana thamani zaidi ya hizo zawadi.

Mabibi na Mabwana,

Nimalizie kwa kupongeza juhudi zinazofanywa za kuboresha makuzi ya vijana haswa mtoto wa kike. Haya ni masuala muhimu sana, ndio maana tuliunda Taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA). Uboreshaji wa afya ya uzazi na elimu kwa mtoto wa kike, ni baadhi ya mikakati ya kipaumbele ya WAMA. Aidha, Taasisi ya WAMA imekuwa ikisaidiana na mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi kwa kujenga shule za mfano kama ile ya WAMA Nakayama, na mabweni kwa ajili ya kuwahifadhi watoto wa kike ili wapate elimu bora na kuwawezesha watoto kuwepo shuleni kwa muda mrefu.

Takwimu imetuonesha kuwa mtoto wa kike akikaa shuleni kwa muda mrefu, hupunguza uwezekano wa kupata mimba za utotoni, VVU na ndoa za utotoni. Pia tumekuwa tukitoa Elimu kwa waandishi wa habari pamoja na wananchi juu ya VVU, afya ya uzazi na uzazi salama.

Shukrani na pongezi zangu za dhati nazitoa tena kwa USAID na Engender Health kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusaidia afya ya uzazi miongoni mwa vijana wetu. Nawapongeza walimu kwa kazi nzuri ya kuwatayarisha vijana, pia kamati ya maandalizi kwa maandalizi mazuri ya tamasha hili. Tuwapigie makofi.

Wito wangu kwako msichana J3 iwe ndio DIRA yako.

Nafurahi kutamka kwamba Kampeni ya *"**Jilinde Utimize Ndoto Yako**"* imezinduliwa rasmi.

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA!

MUNGU IBARIKI TANZANIA,

MUNGU WABARIKI VIJANA WOTE WA TANZANIA.